**SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI ZANZIBAR PAMOJA NA KUWEZESHA USHAJIHISHAJI NA UENDELEZAJI WA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Matumizi.

3. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI, ZANZIBAR


4. Kuanzishwa kwa Wakala.

5. Uwezo wa Wakala.

6. Muhuri wa Wakala.

7. Kazi za Wakala.


### SEHEMU YA TATU
### UONGOZI NA UTAWALA WA WAKALA


8. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala.

9. Majukumu ya Mkurugenzi Mkuu.

10. Wafanyakazi wa Wakala.

11. Bodi ya Wakurugenzi.

12. Muda wa Wajumbe wa Bodi.

13. Utaratibu wa vikao vya Bodi.

14. Kujiuzulu kwa Mjumbe wa Bodi.

15. Nafasi ya Mjumbe kuwa wazi.

16. Katibu wa Bodi.

17. Posho kwa Wajumbe.

18. Uwezo wa Bodi.

19. Kazi za Bodi.

20. Kamati za Bodi.

21. Marufuku ya kutangaza au kutoa taarifa kwa mtu asiye na mamlaka.

22. Fedha za Wakala.

23. Makadirio.

**SEHEMU YA NNE**
**MFUKO WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI**

24. Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

25. Usimamizi wa Mfuko.

26. Matumizi ya fedha za Mfuko.

27. Ripoti za hesabu.

**SEHEMU YA TANO**
**VIFUNGU VYA FEDHA**


28. Bajeti ya mwaka na Bajeti ya ziada.

29. Ukaguzi wa hesabu.

30. Taarifa ya mwaka ya Mkurugenzi Mkuu.


**SEHEMU YA SITA**
**MASHARTI MENGINEYO**


31. Waziri kutoa maelekezo ya Kisera kwa Bodi.

32. Usajili wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

33. Makosa na adhabu.

34. Kinga.

35. Kanuni.


**JADWELI**

SHERIA NAMBA 2 YA 2018

NIMESAINI

{DR. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

2 Januari, 2018

# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI ZANZIBAR PAMOJA NA KUWEZESHA USHAJIHISHAJI NA UENDELEZAJI WA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar ya mwaka 2017 na itaanza kutumika mara tu itakapotiwa saini na Rais.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika katika ushajihishaji na uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati, Zanzibar.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maudhui yatahitaji vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria hii;

"mradi" kuhusiana na miradi ya kati na midogo au midogo midogo, maana yake ni miradi inayoendeshwa kibiashara inayohusiana na utengenezaji, usarifu, ukamuzi, uzalishaji, kilimo, usarifu wa mazao ya kilimo, utalii, biashara ya jumla na rejareja, miradi inayotoa huduma, viwanda vidogo au vinavyofanya shughuli zao nyumbani, kusafirisha bidhaa nje ya nchi na shughuli nyengine za viwanda au biashara;

"mradi au kiwanda" maana yake ni mradi ulioanzishwa au unaoendeshwa na kikundi cha watu, mtu mmoja au taasisi, ambao unafanya biashara, au unazalisha bidhaa au kutoa huduma kwa ajili ya kupata faida;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala ambae ameteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii;

"mradi wa kati au kiwanda cha kati" maana yake ni mradi au kiwanda chochote chenye jumla ya rasilimali zenye thamani inayozidi shilingi za kitanzania milioni hamsini na saba (TZS 57,000,000) lakini isiyozidi shilingi za kitanzania milioni mia sita na hamsini (TZS 650, 000,000) au chenye wafanyakazi wasiopungua ishirini na wasiozidi tisini na tisa;

"mradi mdogo mdogo au kiwanda kidogo kidogo" maana yake ni mradi au kiwanda chochote chenye jumla ya rasilimali zenye thamani isiyozidi shilingi za kitanzania milioni kumi na moja (TZS 11,000,000) au chenye wafanyakazi wasiozidi wanne;

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya viwanda;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya viwanda;

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati ambayo imeundwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"sekta binafsi" maana yake ni mtu, au kikundi cha watu au umoja wa watu wanaojihusisha na miradi au masuala mengine ya maendeleo, wanaofanya shughuli hizo ndani ya Zanzibar, na ambapo mmiliki mkubwa zaidi wa hisa katika shughuli hizo siyo Serikali;

"mradi mdogo au kiwanda kidogo" maana yake ni mradi au kiwanda chochote chenye jumla ya rasilimali zenye thamani inayozidi shilingi za kitanzania milioni kumi na moja (TZS 11,000,000) lakini isiyozidi

shilingi za kitanzania milioni hamsini na saba TZS (57,000,000) au chenye wafanyakazi wasiopungua watano na wasiozidi kumi na tisa.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Wakala.

**4.**-(1) Kunaanzishwa Wakala wa Serikali inayojulikana kama Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar, ambayo kwa ufupisho wake ni SMIDA.

(2) Wakala itakuwa ni chombo cha Serikali kisichojitegemea kikamilifu na kwa idhini ya Waziri na kwa kutumia jina lake itakuwa na uwezo wa:

(a) kupokea kama dhamana, kununua au kwa namna nyengine, kupata, kumiliki, kutoza au kuondoa mali inayohamishika na isiyohamishika;

(b) kuingia mikataba na miamala kwa mujibu wa Sheria; na

(c) kufanya yale yote yatakayoonekana kuwa ni ya lazima, yenye tija au kufaa kufanywa katika utekelezaji bora wa majukumu ya Wakala kwa mujibu wa Sheria na ambayo kwa kawaida hufanywa na chombo kama hiki.

Uwezo wa Wakala.

**5.** Wakala itakuwa na uwezo wa:

(a) kununua, kubadilishana, kukodi au, kwa namna nyengine, kupata mali inayohamishika au isiyohamishika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake;

(b) kutayarisha mikataba au kuchukua dhamana kwa mambo yanayohusiana na utekelezaji wa kazi za Wakala, na kuifanyia marekebisho au kuifuta mikataba au dhamana hizo;

(c) kushirikiana au kuingia katika ubia au ushirika na mtu yeyote au ushirika na watu wanaofanya au wanaojishughulisha na miradi ya kibiashara inayoweza kutekelezwa moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja kwa ajili ya maslahi ya Wakala;

(d) kukopesha au kuazima pesa, au kuwa na maslahi, kuchukua dhamana au kwa namna nyengine yoyote, kusaidia katika upatikanaji wa mitaji kwa miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(e) kutoa, au kuingia katika makubaliano ya kutoa, ushauri kuhusu uendeshaji wa miradi kwa mtu ambae Wakala utaona anashughulika au anatarajia kushughulika na mradi wowote wa viwanda;

(f) kutoa, au kuingia katika makubaliano ya kutoa, mafunzo mahsusi ya uendeshaji wa miradi ya viwanda;

(g) kuajiri wafanyakazi, kwa idhini ya Bodi, na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(h) kuwalipa mafao, mishahara, marupurupu, na posho wafanyakazi wa Wakala kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Muhuri wa Wakala.

**6.** Kutakuwa na muhuri rasmi wa Wakala katika umbo na ukubwa ambao utaamuliwa na Bodi.

Kazi za Wakala.

**7.** Wakala itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kubuni na kutekeleza mipango ya kusaidia maendeleo ya miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo,Vidogo na vya Kati;

(b) kushajihisha uanzishaji na kuendeleza miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(c) kutoa ushauri, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utendaji wa miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(d) kuanzisha, kuendesha au kuwezesha upatikanaji wa huduma za mikopo yenye masharti nafuu na huduma nyengine za kifedha na zisizo za kifedha kwa ajili ya miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(e) kuishauri Serikali kwa mambo yote yanayohusu maendeleo ya miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(f) kuratibu na kuchangia katika tafiti za masoko kwa bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(g) kuwezesha mipango bora ya maendeleo ya miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati mikoani na vijijini kwa kushajihisha matumizi ya taaluma, stadi na rasilimali zinazopatikana katika maeneo hayo;

(h) kuimarisha uwezo wa kushindana wa bidhaa za miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati kwa kuwapatia wahusika wa miradi hiyo misaada ya kiufundi;

(i) Kutoa na kuhimiza upatikanaji wa huduma za mafunzo kwa watu walioajiriwa au wanaotarajia kuajiriwa katika miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(j) kutoa huduma za kiutawala na ushauri kwa miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(k) kuimarisha viwango vya bidhaa na ubora kwa kuzingatia maendeleo na matumizi bora ya teknolojia, vifungashio, ubunifu wa bidhaa na katika huduma za ufundi;

(l) kutoa maeneo bora yenye miundombinu mizuri ya kufanyia kazi kwa gharama nafuu ikiwemo maeneo ya kuendeleza teknolojia na majengo yaliyotengwa kwa ajili ya uzalishaji;

(m) kuwezesha miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati kupata vifaa mwafaka vya kufanyia kazi zao ama kwa njia ya kununua, kukodi au kwa makubaliano ya kibiashara;

(n) kutoa huduma za kiufundi kupitia karakana za mekanika na umeme zinazoendeshwa na Wakala;

(o) kuwezesha upatikanaji wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa kwa bidhaa na huduma za miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(p) kuratibu, kuoanisha na kuwezesha shughuli, miradi na mipango ya pamoja ya maendeleo ya taasisi mbalimbali za umma na za binafsi kuhusiana na miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(q) kupendekeza kwa Waziri vivutio vitakavyoshajihisha uanzishwaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati pamoja na kupendekeza mbinu muafaka za kuvilinda Viwanda hivyo.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI NA UTAWALA WA WAKALA

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala.

**8.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala ambae atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ni:

(a) Mzanzibari;

(b) mwenye angalau Shahada ya Kwanza au inayolingana nayo kutoka Chuo kinachotambulika katika fani ya Uhandisi, Utawala wa Biashara, Uchumi au Uendeshaji wa Viwanda; na

(c) mwenye uzoefu wa angalau miaka mitano katika masuala ya maendeleo ya miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na ujasiriamali.

Majukumu ya Mkurugenzi Mkuu.

**9.** Mkurugenzi Mkuu atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala na atawajibika kuongoza na kusimamia kazi za kila siku na utawala wa Wakala;

(b) atabuni, ataendeleza na kutekeleza mikakati ya kukuza ujasiriamali wa viwanda kwa idhini ya Bodi;

(c) atashirikiana na taasisi zinazotoa mafunzo katika kuandaa mipango ya mafunzo kwa wajasiriamali wa viwanda;

(d) atawasiliana na taasisi za kiufundi na za kifedha, taasisi zinazosaidia miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati, vyombo vya Serikali na mashirika ya kikanda na ya kimataifa ili kutafuta rasilimali za kiufundi na za kifedha kwa ajili ya maendeleo ya miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati, baada ya kupata idhini ya Bodi na ruhusa ya Wizara inayosimamia mambo ya fedha;

(e) atakabiliana na tatizo lolote ambalo linaonekana kikwazo kwa maendeleo ya Viwanda kwa idhini ya Bodi.

Wafanyakazi wa Wakala.

**10.**-(1) Bodi kwa kuzingatia mapendekezo ya Mkurugenzi Mkuu, inaweza kuajiri wafanyakazi wengine wa Wakala au kumkodi mtu kufanya kazi ya ushauri elekezi au mtaalamu kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Wakala.

(2) Uajiri wa wafanyakazi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utafanywa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Wafanyakazi waliopo wa Idara wataendelea kufanya kazi na watachukuliwa kuwa ni wafanyakazi wa Wakala chini ya masharti ya Sheria hii.

(4) Wakala inaweza, kwa kutumia fedha zake, kuandaa mipango ya kuwasomesha wafanyakazi wake na kufanya mambo yanayohusiana na hayo kwa kadri itakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanikisha utendaji wa kazi zake.

Bodi ya Wakurugenzi.

**11.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati ambayo itakuwa na jukumu la usimamizi wa jumla wa kazi za Wakala.

(2) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambae atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu anayeingia kwa nafasi yake;

(c) Mjumbe mmoja mmoja kutoka Wizara zinazosimamia Viwanda, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Uwezeshaji wa Miradi Midogo Midogo, Midogo na ya Kati na wajasiriamali; na

(d) Wajumbe wawili kutoka jumuiya au taasisi za sekta binafsi wanaoshughulika na uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

(3) Wajumbe waliotajwa katika vifungu vidogo vya 2(c) na (d) vya kifungu hiki watateuliwa na Waziri baada ya mashauriano na taasisi husika.

(4) Makamu Mwenyekiti atateuliwa na Bodi kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi.

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**12.**-(1) Mwenyekiti atatumikia ofisi kwa muda wa miaka minne kuanzia tarehe ya uteuzi wake na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

(2) Ukiacha Mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Wajumbe wengine wa Bodi watatumikia nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi na wanaweza kuwa na sifa ya kuteuliwa tena.

13. Utaratibu wa vikao vya Bodi utakuwa kama utakavyoelezwa katika Jadweli la Sheria hii.

Utaratibu wa vikao vya Bodi.

Kujiuzulu kwa mjumbe wa Bodi.

**14.**-(1) Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Bodi anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa notisi ya maandishi kwa Mamlaka iliyomteuwa, na kuanzia siku iliyoainishwa kwenye notisi, au kama tarehe haikuainishwa, kuanzia tarehe iliyopelekewa notisi katika mamlaka ya uteuzi, atasita kuwa mjumbe.

(2) Mtu atakaposita kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi vyovyote itakavyokuwa, kwa sababu yoyote, kabla ya kumalizika muda wake wa utumishi wa Bodi, Mamlaka ya uteuzi itamteuwa mtu mwengine kushikilia nafasi hiyo na mtu huyo aliyeteuliwa atashikilia ofisi kwa muda uliobaki wa mtangulizi wake.

Nafasi ya Mjumbe kuwa wazi.

**15.**-(1) Nafasi ya mjumbe itakuwa wazi iwapo mjumbe huyo:

(a) amefariki;

(b) hakuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya udhuru unaokubalika wakati mjumbe huyo alikuwa na taarifa ya vikao hivyo;

(c) amekoma kuwa mwakilishi wa Taasisi iliyomteua;

(d) amejiuzulu; au

(e) amepoteza uwezo wa kutekeleza majukumu yake, kimwili au kiakili.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii kuhusiana na akidi ya mikutano yake, Bodi inaweza kuendelea na shughuli zake bila ya kujali kutokuwepo kwa mjumbe yeyote, na kitendo chochote kitakachofanyika katika kikao hicho hakitokosa uhalali kwa sababu tu ya kasoro iliyokuwepo kuhusiana na uteuzi wa mtu ambae amekusudiwa kuwa ni mjumbe.

Katibu wa Bodi.

**16.**-(1) Bodi itamteuwa Afisa Sheria mwenye angalau Shahada ya Kwanza katika fani ya Sheria na mwenye uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu kuwa katibu wa Bodi.

(2) Pamoja na kazi nyengine atakazopewa na Bodi, Katibu ana jukumu la kuhakikisha kuwa:

(a) anaweka na kutunza vyema taarifa sahihi za kumbukumbu ya mikutano ya Bodi;

(b) kumbukumbu sahihi na zinazojitosheleza za Bodi zinatunzwa kwa umakini;

(c) anatoa taarifa kwa wajumbe kwa wakati muafaka kuhusiana na mikutano ya Bodi;

(d) anatoa ushauri muafaka kwa Bodi pale inapohitajika; na

(e) anafanya kazi nyengine yoyote atakayoelekezwa na Bodi.

(3) Endapo Katibu hayupo au hawezi kufanya kazi zake kwa sababu ya ugonjwa au kutokana na sababu nyengine yoyote, Bodi itamchagua mfanyakazi yeyote wa Wakala mwenye sifa zinazofaa kutekeleza kazi za Katibu kwa muda wote wa kutokuwepo au kushindwa kufanya kazi mpaka Katibu husika atakaporejea katika nafasi yake au atakapoteuliwa Katibu mwengine.

Posho kwa wajumbe.

**17.** Mwenyekiti, Mjumbe wa Bodi au wa kamati yoyote ya Bodi, atapewa posho na malipo mengine kama itakavyopangwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Uwezo wa Bodi.

**18.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, usimamizi wa jumla na miongozo ya Kisera kuhusiana na uendeshaji wa kazi za Wakala vitakuwa chini Bodi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi itakuwa na mamlaka ya:

(a) kutoa miongozo ya kimkakati kwa Wakala katika kutekeleza kazi zake;

(b) kusimamia kazi za Wakala kuhusiana na kukuza, kuchochea, kuwezesha na kuimarisha maendeleo ya sekta ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(c) kutoa idhini ya kupelekwa taarifa za Wakala kwa Waziri;

(d) kusimamia mali zote zinazohamishika na zisizohamishika, Mfuko wa Maendeleo wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na mali nyengine za Wakala;

(e) kuidhinisha bajeti ya mwaka na bajeti ya ziada, pamoja na mipango na miongozo ya Wakala;

(f) kuweka viwango vya ada pamoja na tozo nyengine zinazostahiki kulipwa kutokana na huduma zinazotolewa na Wakala;

(g) kuagiza kupatiwa taarifa au kumbukumbu zinazohusiana na jambo lolote la ujasiriamali wa viwanda lililoamuliwa na Wakala; na

(h) kuchukua hatua za kinidhamu kwa wafanyakazi wa ngazi ya juu wa Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kazi za Bodi.

**19.**-(1) Bodi itakuwa na kazi za kushajihisha na kuwezesha maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na kuweka mazingira bora kwa ajili ya kufikia lengo lililokusudiwa,

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kutoa maelekezo yanayokubalika kisheria kwa Mkurugenzi Mkuu juu ya masuala ya utawala, utendaji na Sera za uendeshaji wa Wakala;

(b) kuanzisha muundo wa Wakala kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma na kuweka utaratibu wa utendaji kazi kwa kadri itakavyoonekana inafaa kwa madhumuni ya kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Wakala;

(c) kwa idhini ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma, kuweka miongozo na masharti yanayohusiana na utumishi, mishahara na maposho mengine ikiwemo maslahi mengine kwa waajiriwa wa Wakala;

(d) kuweka mikakati, mipango kazi, makusudio na malengo muafaka ya kazi ya kila Idara ya Wakala na kufuatilia kwa mfululizo maendeleo yanayotokana na mambo yaliyopangwa katika kufikia malengo hayo;

(e) kwa idhini ya Waziri, kuweka Sera za utekelezaji wa Wakala;

(f) kuzingatia, kuidhinisha na kufuatilia utekelezaji wa bajeti za mwaka na za robo mwaka za Wakala;

(g) kufuatilia kwa makini usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(h) kuandaa na kuzisimamia kanuni za wafanyakazi na za fedha;

(i) kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wakala;

(j) kuishauri Serikali kupitia Waziri kuhusiana na mambo yanayohusu uendelezaji wa Wakala; na

(k) kufanya kazi nyengine ambazo kwa kawaida zinafanywa na Bodi.

Kamati za Bodi.

**20.**-(1) Bodi inaweza kuanzisha kamati mbali mbali kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii na inaweza kukasimu kazi yoyote katika kamati yoyote kwa kadri itakavyoona inafaa.

(2) Bodi inaweza kuteua wajumbe wa kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki miongoni mwa wajumbe wa Bodi.

(3) Kamati za Bodi zinaweza kumualika mtu yeyote kushiriki katika vikao vyake, lakini mtu huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

(4) Kwa kuzingatia maelekezo maalum au ya jumla ya Bodi, Kamati yoyote iliyoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki inaweza kujiwekea utaratibu wake.

(5) Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalum kwa kadri Bodi itakavyoamua.

(6) Utaratibu wa vikao, mambo muhimu na mengineyo kuhusiana na kamati hizo zitakazoanzishwa yatawekwa na Bodi.

Marufuku ya kutangaza au kutoa taarifa kwa mtu asiye na mamlaka.

**21.**-(1) Ni marufuku kwa Mjumbe wa Bodi, mfanyakazi wa Wakala, mtu yeyote aliyealikwa kuhudhuria kikao cha Bodi au kamati yoyote ya Bodi, bila idhini ya maandishi iliyotolewa na Bodi au iliyotolewa kwa niaba ya Bodi, kutangaza au kutoa taarifa kwa mtu yeyote ikiwemo maandishi ya waraka, mawasiliano au taarifa na mengine kama hayo yanayohusiana au anayoyafahamu katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii, isipokuwa kwa yule ambaye anatekeleza wajibu wake kisheria.

(2) Mtu ambae atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, amefanya kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiopungua miezi sita na usiozidi miaka miwili au vyote viwili.

Fedha za Wakala.

**22.** Fedha za Wakala zitajumuisha:

(a) Fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kila mwaka wa fedha;

(b) Misaada, bakaa, mikopo na michango mingine ya fedha kutoka Serikalini, au kwa mtu mwengine au kutoka vyanzo vyengine vinavyokubalika kwa idhini ya Waziri; na

(c) Fedha zozote halali ambazo zitapokelewa na zitakazopatikana kwa Wakala.

Makadirio.

**23.** Mkurugenzi Mkuu atatayarisha taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wakala kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha kwa ajili ya mwaka unaofuata, na kuyawasilisha kwa Waziri baada ya kuthibitishwa na Bodi kwa kuingizwa katika Bajeti ya Wizara.

## SEHEMU YA NNE
## MFUKO WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI

Mfuko wa maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

**24.**-(1) Kunaanzishwa Mfuko, kwa idhini ya Waziri anayehusika na Fedha, unaojulikana kama Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

(2) Mfuko ulioanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utatumika kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

(3) Vyanzo vya Fedha za Mfuko vitajumuisha:

(a) Fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kila mwaka wa fedha;

(b) Misaada, bakaa, mikopo na michango mingine ya fedha kutoka Serikalini, au kwa mtu mwengine au kutoka vyanzo vyengine vinavyokubalika kwa idhini ya Waziri; na

(c) Fedha zozote halali ambazo zitapokelewa na zitakazopatikana kwa Wakala.

Usimamizi wa Mfuko.

**25.**-(1) Mfuko utakuwa chini ya dhamana ya Bodi ya Wakala na utasimamiwa na Mkurugenzi Mkuu kwa mujibu wa maelekezo yatakayotolewa na Bodi kila baada ya muda.

(2) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazoeleza namna na taratibu za matumizi ya fedha za Mfuko.

Matumizi ya fedha za Mfuko.

**26.** Fedha za Mfuko zitatumika kwa:

(a) kufanya tafiti kwa ajili ya uhamasishaji na maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(b) upatikanaji wa ardhi, zana, vifaa mbali mbali, mali nyengine na ujenzi wa majengo kwa ajili ya kukuza malengo ya mfuko;

(c) upatikanaji wa majengo bora na kwa bei nafuu kwa ajili ya utendaji kazi yenye miundo mbinu imara yakiwemo maeneo ya kuendeleza teknolojia na majengo yaliyotengwa kwa ajili ya uzalishaji;

(d) kutoa huduma za kiufundi kupitia karakana za mekanika na umeme au nyenzo na vifaa vya kiufundi vinavyoendeshwa na Wakala;

(e) kuanzisha, kuendesha na kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu na huduma nyengine za kifedha na zisizo za kifedha kwa ajili ya maendeleo ya viwanda;

(f) kutoa mikopo au misaada kwa taasisi yoyote ambayo kwa maoni ya Bodi taasisi hiyo ipo kwa ajili ya kuhamasisha uanzishaji au maendeleo ya shughuli za usarifu na utengenezaji wa bidhaa;

(g) kuviwezesha Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati kupata vifaa stahiki kwa kununua, kukodi au kwa njia nyengine ya makubaliano ya kibiashara kwa kutumia nembo au utaalamu maalum;

(h) kuzikabili gharama zinazotokana na uanzishaji na uendeshaji wa Mfuko;

(i) kwa madhumuni yoyote ambayo kwa maoni ya Bodi, madhumuni hayo yatasaidia kuhamasisha uanzishwaji na maendeleo ya sekta ya ujasiriamali wa viwanda.

Ripoti za hesabu.

**27.** Bodi, ndani ya miezi sita baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, itatayarisha au itawezesha kutayarishwa ripoti ya hesabu za mwaka zilizokaguliwa, zinazohusiana na Mfuko wa maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na kuwasilisha kwa Waziri.

## SEHEMU YA TANO
## VIFUNGU VYA FEDHA

Bajeti ya mwaka na Bajeti ya ziada.

**28.**-(1) Bodi itaipitia kwa makini Bajeti ya mwaka sambamba na makadirio ya kiwango kilichotarajiwa kupokelewa na kutumiwa na Wakala katika mwaka wa fedha, katika muda ambao si chini ya miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha.

(2) Iwapo katika mwaka wowote wa fedha, Wakala itahitaji kufanya matumizi ambayo hayakuelezwa katika Bajeti ya mwaka, Bodi itafanya kikao na kuzingatia

Bajeti hiyo ya ziada inayoelezea kwa umakini matumizi yanayohitajika na kuwasilisha kwa Waziri ili kupata idhini.

(3) Iwapo Bodi imeidhinisha Bajeti ya mwaka au bajeti ya ziada, bajeti hiyo ya mwaka au bajeti ya ziada, vyovyote itakavyokuwa, itakuwa ni lazima kwa Wakala kufanya matumizi yake kwa mujibu wa makadirio yaliyowekwa katika Bajeti hiyo iliyoidhinishwa.

Ukaguzi wa hesabu.

**29.**-(1) Wakala itaweka au itawezesha kuwekwa vitabu vya hesabu na kumbukumbu za fedha zinazohusiana na :

(a) Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati;

(b) Risiti na matumizi ya fedha, na miamala ya kifedha yaliyofanywa na Wakala;

(c) Mali na dhima za Wakala; na

(d) Taarifa za maandishi za kifedha za kila mwaka wa fedha zinazoainisha maelezo kamili kuhusiana na mapato na matumizi ikiwa pamoja na mali iliyopo na dhima kwa Wakala.

(2) Mfuko utafanyiwa ukaguzi katika kila mwaka wa fedha na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi yeyote aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi yeyote aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka huo wa fedha atafanya ukaguzi wa hesabu za Wakala ikiwemo taarifa za maandishi za kifedha zinazohusiana na mwaka wa fedha.

(4) Hesabu zilizokaguliwa zitawasilishwa kwa Bodi na zitakapokubaliwa na kuridhiwa na Bodi zitawekwa muhuri wa kuthibitishwa kuwa zimekubaliwa na kuridhiwa.

(5) Mara baada ya hesabu za Wakala kukaguliwa, na katika hali yoyote isiyo zaidi ya miezi sita baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, Bodi itawasilisha kwa Waziri nakala ya hesabu zilizokaguliwa sambamba na nakala ya taarifa ya ukaguzi iliyoandaliwa na Mkaguzi.

Taarifa ya mwaka ya Mkurugenzi Mkuu.

**30.** Mkurugenzi Mkuu atatayarisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wakala kila ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha na kuiwasilisha kwa Waziri baada ya kupata idhini ya Bodi.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Waziri kutoa maelekezo ya Kisera kwa Bodi.

**31.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Waziri anaweza kutoa maelekezo ya jumla ya kisera kuhusiana na uendeshaji wa Wakala au kuhusiana na utekelezaji bora wa kazi za Bodi au kazi na malengo ya Wakala.

Usajili wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati.

**32.** Mtu anayeanzisha au anayefanya mradi wa kiwanda Zanzibar atalazimika kufanya usajili kwa mujibu wa Sheria inayohusiana na Usajili wa Taasisi za Biashara.

Makosa na adhabu.

**33.**-(1) Mtu atakayempa taarifa au maelezo Waziri, mjumbe wa Bodi au wa kamati ya Bodi au Mkurugenzi Mkuu, hali akijua kuwa taarifa au maelezo hayo ni ya uongo, ametenda kosa.

(2) Mtu atakayeshindwa kutekeleza agizo lolote au amri halali iliyoamriwa chini ya Sheria hii, ametenda kosa.

(3) Mtu anyaemzuia mjumbe wa Bodi, mjumbe wa kamati ya Bodi, au mfanyakazi wa Wakala kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii, ametenda kosa.

(4) Mtu anayekwenda kinyume na sharti lolote chini ya Sheria hii ametenda kosa.

(5) Mtu aliyetiwa hatiani chini ya vifungu vidogo vya (1), (2), (3) au (4) vya kifungu hiki atalazimika kulipa faini ya shilingi za kitanzania zisizopungua milioni moja na zisizozidi milioni tatu, au kifungo cha muda usiozidi mwaka mmoja au vyote viwili.

(6) Mtu yeyote mwenye taarifa ambazo kwa ufahamu wake zimechapishwa au zimetolewa kwa mujibu wa ukiukwaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, na bila ya halali akazisambaza au kuziwasilisha taarifa hizo kwa mtu mwengine, ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalazimika kulipa faini ya shilingi za Kitanzania zisizozidi milioni mbili au kifungo kwa muda usiozidi miezi sita au vyote viwili.

Kinga.

**34.** Mjumbe wa Bodi, au Afisa wa Wakala hatowajibika yeye binafsi kutokana na jambo au kitu chochote kitakachofanywa au kuachwa kufanywa na ikiwa tendo au jambo hilo litafanywa au kuacha kufanywa kwa nia njema katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii.

Kanuni.

**35.** Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kutunga kanuni zinazoelezea:

(i) Mambo yote yanayohitaji au kuruhusika kuelezwa na Sheria hii;

(ii) Fomu yoyote inayohitajika kwa mujibu wa utekelezaji wa Sheria hii;

(iii) Ada yoyote inayohitajika kulipwa kutokana na huduma zinazotolewa na Wakala; au

(iv) Mambo mengine yoyote ambayo ni muhimu na yanayohitajika kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

## JADWELI
## UTARATIBU WA VIKAO VYA BODI
**{Chini ya kifungu cha 13}**

Vikao vya Bodi.

**1.**-(1) Bodi itafanya vikao vyake mara moja katika kipindi cha kila miezi mitatu na itaweza kuitisha mkutano wakati wowote itakapotokezea haja ya kufanya hivyo katika utekelezaji wa kazi zake.

(2) Vikao vya Bodi vitaongozwa na Mwenyekiti, na itakapokuwa Mwenyekiti hayupo kikao kitaongozwa na Makamu Mwenyekiti.

(3) Mwenyekiti au atakapokuwa hayupo, Makamu Mwenyekiti wataitisha mkutano maalum kwa ombi la maandishi litakalosainiwa na zaidi ya nusu ya wajumbe wa Bodi na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti atawezesha mkutano huo kufanyika ndani ya siku ishirini na moja kuanzia siku ya kupokea ombi hilo.

(4) Iwapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wote hawapo, wajumbe waliopo watamteuwa mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao, na mjumbe aliyechaguliwa atakuwa na uwezo na kutekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti.

Akidi ya kikao.

**2.** Akidi ya kikao cha Bodi ni zaidi ya nusu ya wajumbe.

Maamuzi ya Bodi.

**3.**-(1) Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa makubaliano ya pamoja na ikiwa makubaliano hayatofikiwa, maamuzi yatafanyika kwa kupiga kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi inaweza kufanya maamuzi kwa kusambaza waraka kwa wajumbe na kila mjumbe akaweza kutoa maoni yake kwa maandishi, isipokuwa kwamba mjumbe yeyote anaweza kuomba maamuzi hayo kupelekwa mbele kwa ajili ya mjadala kwenye kikao kamili cha Bodi.

(3) Maazimio yaliyotolewa kwa maandishi kwa wajumbe waliopo Zanzibar ambao si chini ya wajumbe watano, yatakubalika kuwa ni maamuzi sahihi kama maamuzi yanayofanywa katika vikao vya kawaida vya Bodi, isipokuwa kwamba, mjumbe, bila ya kuathiri saini yake katika maamuzi hayo, anaweza kuomba maamuzi hayo kupelekwa mbele kwa ajili ya mjadala kwenye kikao kijacho cha Bodi.

Mualikwa katika Bodi.

**4.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kutoa ushauri katika kikao chake chochote lakini mtu huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbukumbu za vikao vya Bodi.

**5.** Kumbukumbu za kila kikao cha Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao chake kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti pamoja na Katibu wa Bodi.

Utaratibu wa vikao.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kujiwekea utaratibu wa uendeshaji wa vikao vyake na mwenendo bora wa shughuli zake ikijumuisha kamati za Bodi.

Kuweka bayana mgongano wa maslahi.

**7.** Mtu yeyote ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au ya aina yoyote ile katika agenda au jambo litakaloamuliwa katika kikao cha Bodi, atalazimika kuweka bayana katika Bodi uwepo wa maslahi hayo na hatopaswa kushiriki katika maamuzi yanayohusiana na ajenda au jambo hilo.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar tarehe 7 Disemba, 2017.

.................................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***
***Zanzibar.***